**FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL13**

**KISWAHILI PAPER 3 QUESTIONS**

## 1. SEHEMU YA A (Alama 20 )

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

1\. 1. Naja sasa njiyani, naja kwetu mzalendo
Naja nirudi nyumbani, nilowekwa nako kando
Kwetu ni nakutamani, kulo na mwingi uhondo
Nifanye ni ile nyundo, misumari hadharini.

2\. Naja kwingine kuwapi, kulojaa langu pendo,
Nenda nende kwinginepo, sawa nako kwa muundo
Kaa kwingine anapo, ela kwenye lakwe gando
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini.

3\. Naja nije rudi papo, panigandane mgambo
Ningaambiwa kwetu hapo, kwamba kwanuka uvundo
Sitakwenda penginepo, tayari kuko kwa mwando
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini.

4\. Naja sitapakimbiya, ningambwa kuna uvundo
Takuja kuvielekeya, vingajiya kwa vundo
Nilipozawa tafiya, sikimbii kweanda kando
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini.

5\. Naja kiwa mikomaa, kuzidi nilvyo mwando
Tena najiandaa, kwa fikira na vitendo
Kwetu nije kuifaa, na kuitiliya pondo
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini.

6\. Naja na lagawa siwaekei mifundo
Moyo wangu ushatuja, mawi nalotendewa mwando
Ela watuoningoja, na hivyo vitendo.
Nijaye ni ile nyundo,musumari hadharini

a) Lipatie shairi hili kichwa mwafaka. (Al.2)

b) Onyesha jinsi kanuni za utunzi zilivyotumiwa kusanifu shairi hili.(Al.5)

c) Kwa kutoa mifano mwafaka eleza jinsi uhuru wa kishairi ulivyotumiwa. (Al. 5)

d) Taja na ueleze mbinu inayopatikana katika ubeti wa tatu. (Al.2)

e) Eleza ujumbe unaopatikana katika ubeti wa pili mshororo wa tatu.(Al.2)

f) Andika ubeti wa sita kwa lugha nathari. (Al. 4)

g) Andika maneno haya kwa lugha sanifu. (Al.2)

i) Mwando.

ii) Ningambwa.

## 2 .SEHEMU YA B (Alama 20 )

**2.** a) Jadili mbinu mbalimbali walizotumia Wanacheneo kupinga dhuluma. (Al.10)

b) Jadili uozo wa kijamii unaojitokeza katika jamii ya Cheneo. (Al. 10)

**3.** **AU**

Jadili matumizi ya mbinu zifuatazo. (Al.20)

i) Kinaya

ii) Mbinu rejeshi

iii) Taharuki

iv) Uzungumzi nafsia

v) Nyimbo

## 3.SEHEMU YA C (Alama 20 )

**4.** Kwa kurejelea hadithi zozote tano, jadili matatizo yanayowakumba vijana katika jamii. (Al.20)

**5.** **AU**

5. "Nani amekwambia kwamba mimi unanihusudu? Lini nimekulalamikia hivyo au kumlalamikia mtu mwingine…?

i) Eleza mkutadha wa dondoo hili. (Al.4)

ii) Eleza sifa za msemaji wa maneno haya. (Al.6)

iii) Onyesha jinsi msemewa alivyoonyesha uozo katika jamii. (Al.10)

## 4.SEHEMU YA D (Alama 20 )

6. a)

i) Ni nini maana ya ngomezi. (Al.2)

ii) Fafanua sifa tano za ngomezi. (Al.5)

iii) Taja mifano mitatu ya ngomezi ya kisasa. (Al.3)

b)

i) Bainisha aina nne za watendaji wa fasihi simulizi. (Al.4)

ii) Eleza sifa sita bainifu za mtendaji fasihi simulizi (Al.6)

## 5. KIDAGAA (Alama 20 )

7. Eleza ufaafu wa anwani "Kidagaa Kimemwozea" (Al.20)

8. "Lakini one day muwapo wadosi msinisahau mwenzetu….?

a) Bainisha muktadha wa dondoo hili. (Al.4)

b) Licha ya kuchanganya ndimi ni mbinu gani ya uandishi imetumiwa hapa. (Al.4)

c) Wahusika wanaolengwa waliipokeaje kauli hili? (Al.4)

d) Mhusika anayenena hapa hana bahati. Jadili. (Al.8)